# BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 29 Septemba, 2022**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa mwaka 2021/2022.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria Ndogo Ndogo kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Sheria Ndogo Ndogo kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2021/2022.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mtaa na Idara Maalum za SMZ:**

125. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mtaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwakuwa wauza maduka ya maeneo ya Maungani na maeneo mengine ya Jimbo la Dimani, hukata leseni ikijumuisha malipo ya uzoaji wa taka ambayo ni shilingi 50,000/-.

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea wahusika kutokwenda kuchukua taka hizo wakati wafanyabiashara wanalipa tena kwa wakati.

(b) Je, kwanini wafanyabishara wanaendelea kutozwa gharama kubwa za leseni za usafi wakati huduma wanayolipia hawaipati.

(c) Je, hatua gani Wizara itachukua ili kurekebisha changamoto hiyo isiendelee tena.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

108. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Wananchi walio wengi na walioathirika na mkasa wa ‘Master Life’ wanatoa shukrani zao za dhati kwa Serikali kwa kuutumia Mfuko Mkuu wa Serikali kuwafidia mitaji yao iliyonyang’anywa na kikundi cha ‘Master Life’. Hata hivyo, bado kuna malalamiko ya kupunjwa au kutolipwa kabisa kwa baadhi ya wananchi hao.

Je, ni hatua ipi Serikali imefikia katika kuwamalizia waathirika madeni yao na katika kurejesha pesa ya Serikali kutoka katika mali za ‘Master Life’.

133. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 imebainika kuyakwaza kiutendaji Mashirika ya Kibiashara.

Je, ni lini Serikali italeta Barazani Mswada wa Marekebisho ya

Sheria hiyo, ili kuondoa changamoto mbali mbali zinazokwamisha utekelezaji wa Sheria hiyo hasa kwa Mashirika hayo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

76. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Inafahamika kwamba, mashirika kadhaa ya ndege yalikuwa na ratiba ya safari za Pemba/Tanga. Hata hivyo, hivi karibuni kumekuwa na upungufu mkubwa wa safari hizo na inasemekana kuwa zimesitishwa, pamoja na ukweli kwamba ratiba za safari hizo ziliwarahisisishia sana wananchi walio wengi kufika Tanga/Pemba kwa urahisi zaidi.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kukatishwa kwa safari hizo.

(b) Je, kuna ugumu gani kwa Serikali yetu kuwashajiisha wamiliki wa ndege kuzirejesha safari hizo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

68. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kama inavyofahamika, sehemu zenye mikoko ni moja kati ya maeneo ambayo samaki hutaga mayai na yanakuwa ndio mazalio ya samaki mbali mbali kama vile kaa, shirima, changu na kolekole. Hata hivyo, kiwango cha kuihifadhi na kuidhibiti mikoko bado hakijaridhisha, ukilinganisha na umuhimu wake.

(a) Je, Serikali, kupitia Wizara yenye dhamana ya Kilimo, inashirikianaje na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi katika kuihifadhi mikoko hiyo.

(b) Je, Serikali imepanga mbadala upi wa kuzuia mikoko inayokatwa kwa kujengewa pamoja na kutengenezewa mkaa.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

116. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Eneo la Kizingo karibu na Hospitali ya Mnazi Mmoja, kuna shughuli za wavuvi na mnada wa samaki za kutwa nzima. Hata hivyo, suala la usalama na utunzaji wa mazingira katika eneo hilo linalooneka hafifu.

(a) Je, Wizara inachukua hatua gani kudhibiti hali hiyo.

(b) Je, ni lini Mhe.Waziri na watendaji wako mtafanya ziara ya kulikagua eneo hilo na kuwapa wavuvi na watumiaji wengine maelekezo ya utumiaji bora wa eneo hilo.

(c) Je, ni lini Serikali itaweka udhibiti wa kujua wanaoingia kupitia bahari ya eneo hilo, ili kuepusha watu wasiokuwa na nia njema kuingia nchini kinyume na sheria.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

89. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madinii:

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wafanyabiashara katika Jumba la Treni Darajani Unguja, kuhusiana na utata katika kulipia maji kwa kiwango kisichoridhisha na kisichostahiki.

Je hivi sasa hali ikoje na upi mpango mpya wa ulipaji wa maji kwa wafanyabiashara wa Jumba la Treni, Darajani Unguja.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

147. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa jimbo la Wawi ni miongoni mwa majimbo yenye skuli kongwe sana, na kwa kuwa baadhi ya skuli hizo zimechakaa na baadhi ya mabanda kuanguka kabisa.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya miradi ya elimu kwa jimbo la Wawi kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023.

(b) Je, ni skuli zipi zitanufaika na fedha hizo.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa mwaka 2021/2022.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2021/2022.

Zanzibar,
29 Septemba, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.